HISTORIA YA HARAKATI ZA WAFANYAKAZI WA TANZANIA KATIKA KUDAI HAKI ZAO KATIKA VIPINDI MBALIMBALI NA MIFUMO TOFAUTI YA KISIASA NA KIUCHUMI[1]

Kipindi (MWAKA) 1950-1960

MFUMO WA VYAMA VYA WAFANYAKAZI	MFUMO WA KISIASA	MFUMO WA UCHUMI NA SERA ZILIZOTUMIKA	MATATIZO KWA WAFANYAKAZI	MBINU ZILIZOTUMIWA NA WAFANYAKAZI KUKABILI MATATIZO	MATOKEO
Vyama vingi vya wafanyakazi kisekta chini ya shirikisho moja la vyama vya wafanyakazi, Tanzania Federation of Labour (TFL) lililoundwa Mwaka 1957.	Vyama vingi vya siasa vilivyokuwa vikipigania uhuru ikiwemo TANU iliyokuja kutawala	❖ Uchumi huria wenye sera ya kuifanya nchi kuwa tegemezi, na kuzalisha zaidi malighafi kwa ajili ya viwanda vya Ulaya na watanganyika ❖ Kutumika kama soko kwa bidhaa za Ulaya	❖ Kulipwa mishahara duni ❖ Ajira za kulazimishwa (forced labour) kama vile: manamba kwenye mshamba ya mikonge na chai. ❖ Kufukuzwa kazi holela bila malipo ❖ Mazigira duni ya kazi ❖ Kuzuiwa kujiunga na vyama vya kazi na siasa	❖ Migomo ❖ Majadiliano kidogo yasiyo rasmi wala kisheria baada ya migomo. ❖ Kujiunga pamoja katika vyama vya wafanyakazi	❖ Wafanyakazi walijenga umoja na mshikamano ❖ Baadhi ya matakwa yao yalitekelezwa.

KIPINDI (MWAKA) 1961-1964

MFUMO WA VYAMA VYA WAFANYAKAZI	MFUMO WA KISIASA	MFUMO WA UCHUMINA SERA ZILIZOTUMIKA	MATATIZO KWA WAFANYAKAZI	MBINU ZILIZOTUMIWA NA WAFANYAKAZI KUKABILI MATATIZO	MATOKEO
Vyama vingi vya wafanyakazi kisekta chini ya shirikisho moja la Vyama vya Wafanyakazi, Tanzania Federation of Labour (TFL) lililoundwa mwaka 1957.	❖ Mfumo wa chama kimoja ulianza. Chama cha TANU kikawa ndiyo chama pekee cha siasa	❖ Uchumi huria uliondeleza kuzalisha malighafi kwa viwanda vya Ulaya na kuendeleza soko la bidhaa za Ulaya. ❖ Pia sera ya Umma kumiliki uchumi ilianza kuandaliwa	❖ Mazingira ya kazi yaliendelea kuwa magumu ❖ Mishahara iliendelea kuwa duni ❖ Baadhi ya watumishi wa serikali hawakuruhusi wa kujiunga na vyama vya wafanyakazi	❖ Migoro ❖ Majadiliano Kidogo yasiyo ya kisheria wala rasmi baada ya migogoro kujitokeza	❖ Wafanyakazi walijenga umoja na mshikamano ❖ Baadhi ya Matakwa yao yalitekelezwa ❖ Mfumo wa vyama vingi na uhuru wawafanyakazi kujiunga na chama chochote cha

[1] Muhtasari wa Mada iliyotolewa na Ndg. John Gonza (Mkurugenzi wa Uchumi na Utafiti: TUCTA) katika kongamano la Kitaifa kuhusu Harakati za Wanyonge za Kutetea Haki za Ardhi na Haki za Binadamu Mei 12 – 13, 2005 Dar es Salaam.

					❖ Wafanyakazi uliondolewa ❖ Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi TFL lilivunjwa mwaka 1964 na NUTA kuundwa kama chombo pekee cha Wafanyakazi.

KIPINDI (MWAKA) 1964-1977

MFUMO WA VYAMA VYA WAFANYAKAZI	MFUMO WA KISIASA	MFUMO WA UCHUMINA SERA ZILIZOTUMIKA	MATATIZO KWA WAFANYAKAZI	MBINU ZILIZOTUMIWA NA WAFANYAKAZI KUKABILI MATATIZO	MATOKEO
Chombo kimoja kinachounganisha Wafanyakazi kilianzishwa (NUTA) kilichowekwa chini yha chama Tawala TANU. Katibu Mkuu wa NUTA alitokana na wajumbe wa Halmashauri Kuu ya chama tawala TANU na alipewa pia wadhifa wa Waziri wwa Kazi katika serikali	❖ Chama kimoja cha siasa TANU	❖ Mfumo wa uchumi wa kupangwa na kusimaiwa na serikali ili kutekeleza siasa ya ujamaa na kujitegemea na njia kuu za uchumi kumilikiwa na Umma. ❖ Mashirika mengine ya Umma yalianzishwa na kutoa ajira kwa Watanzania ❖ Sekta binafsi haikuruhusiwa kukua na kumiliki uchumi	❖ Mazingira ya kazi duni ❖ Mishahara isiyokidhi mahitaji muhimu ya maisha ❖ Wafanyakazi kutokuwa na uhuru wa kujiunga ama kuanzisha Vyama vya Wafanyakazi wanavyovipenda ❖ Kukosa uwakilishi wa Wafanyakazi ❖ Kukosekana kwa demokrasia ya kweli ndani ya Vyama vya Wafanyakazi ❖ Kukiukwa kwa haki za msingi Wafanyakazi za kujiunga na vyama na kuchagua viongozi wao. ❖ Baadhi ya wafanyakazi kufukuzwa kazi kwa uonevu. ❖ Baadhi ya ajira kutolewa kwa	❖ Majadiliano kupitia chama tawala na Wizara ya Kazi kwa vile chama cha Wafanyakazi (NUTA) kilikuwa Jumuiya ya Chama Tawala TANU na Katibu Mkuu wa NUTA alikuwa pia Waziri wa Kazi. ❖ Utafiti na elimu kwa waajiri na serikali juu ya hali halisi ya maisha ya wafanyakazi. ❖ Migomo sehemu za kazi isiyo rasmi. ❖ Kuwafungia ofisi watendaji wakuu wa Mashirika ya Umma. ❖ Kufungua matawi ya chama cha Wafanyakazi sehemu za kazi. ❖ Majadiliano kupitia kwenye vikao vya mabaraza ya wafanyakazi ❖ Kutumia risala ya Mei Mosi kwa Rais kila Mwaka. ❖ Kushinikiza kupitia kwa wafadhili, mashirika ya kimataifa, kama vile; ILO, IMF, WB, ili kuwapa	❖ Wafanya kazi walijenga umoja na mshikamano ❖ Baadhi ya matakwa yao yalitekelezwa ❖ Serikali ilianza kuandaa mazingira ya kuwapa uhuru Wafanya kazi kuunda vyama wanavyopenda.

			upendeleo bila sifa ya jambo lililochangia kufa kwa baadhi ya Mashirika ya Umma na ukosefu wa kazi ❖ Baadhi ya Wafanyakazi kunyimwa haki ya kusoma na kujiendeleza nchi za nje kwa sababu za kisiasa kwa sababu hawakuwa wanachama wa chama tawala.	uhuru na haki za msingi Wafanyakazi na vyama vyao. ❖ Kuwasimamia vyema mahakamani wafanyakazi walioonewa na kufukuzwa kazi.	

KIPINDI (MWAKA) 1978-1990

MFUMO WA VYAMA VYA WAFANYAKAZI	MFUMO WA KISIASA	MFUMO WA UCHUMINA SERA ZILIZOTUMIKA	MATATIZO KWA WAFANYAKAZI	MBINU ZILIZOTUMIWA NA WAFANYAKAZI KUKABILI MATATIZO	MATOKEO
Chombo kimoja kinachounganisha Wafanyakazi (JUWATA)	Chama kimoja cha siasa CCM (Chama cha Mapinduzi)	❖ Mfumo wa uchumi wa kupangwa na kusimamiwa na serikali ili kutekeleza siasa ya ujamaa na kujitegemea na njia kuu za uchumi kumilikiwa na Umma. ❖ Kuanza kwa sera za kurekebisha uchumi zikiwemo za ubinafsishaji, kuvutia wawekezaji wa nchi za nje, soko huria, n.k.	❖ Mazingira duni ya kazi ❖ Mishahara duni ❖ Kupunguzwa kazini. ❖ Kutokuwepo kwa uhuru na haki za wafanyakazi kuunda ama kujiunga na chama chochote cha wafanyakazi. ❖ Kutokushirikishwa katika mipango na sera za uchumi na Maendeleo ya nchi. ❖ Kutokuwepo kwa uwakilishi wa kweli wa Wafanyakazi katika vyombo vya maamuzi. ❖ Waajiri wageni/wa sekta binafsi kuanza kuwapuuza Wafanyakazi kwa kutoheshimu sheria za kazi, kuziuia kuanzishwa vyama vya Wafanyakazi sehemu zao za kazi, kuajiri vibarua zaidi, kulipa mishahara duni, kufukuza kazi ovyo, n.k.	❖ Kufanya tafiti na kuzisambaza kwa njiaya machapisho , semina, mikutano. ❖ Kufanya Majadiliano na waajiri na serikali ❖ Migomo isiyo rasmi ❖ Kupeleka malalamiko na maombi maalum serikalini. ❖ Kutumia shinikizo kwa serikali kupitia kwa mashirikisho huru ya Wafanyakazi duniani, ILO, na wafadhili. ❖ Kudai uhuru wa Vyama vya Wafanyakazi kwa wanachama wake, Mahakama ya kazi na kwingineko.	❖ Vyama vya wafanyakazi kuondolewa katika himaya ya chama tawala na kuanchwa huru. ❖ Vyama vya Wafanyakazi kuanza kushirikishwa katika nyanja mbalimbali za Maendeleo. ❖ Kuanza kuonekana uwakilishi wa kweli wa Wafanyakazi sehemu mbalimbali ndani na nje ya nchi.

KIPINDI (MWAKA) 1990-2000

MFUMO WA VYAMA VYA WAFANYAKAZI	MFUMO WA KISIASA	MFUMO WA UCHUMINA SERA ZILIZOTUMIKA	MATATIZO KWA WAFANYAKAZI	MBINU ZILIZOTUMIWA NA WAFANYAKAZI KUKABILI MATATIZO	MATOKEO
Chombo kimoja kinachounganisha Wafanyakazi (OTTU) kilichokuwa huru bila kuwa chini ya chama tawala wala serikali.	Nyama vingi vya siasa	Mfumo wa uchumi wa soko huria na sera za ubinafsishaji ziliendelea	❖ Mazingira duni ya kazi ❖ Mishahara duni ❖ Kutotekelezwa kikamilifu Uhuru na haki za binadamu zikiwemo haki za Wafanyakazi kuunda ama kujiunga na chama chochote cha Wafanyakazi. ❖ Kutokushirikishwa kikamilifu katika mipango na sera za uchumi na aendeleo ya nchi ❖ Uwakilishi mdogo wa Wafanyakazi katika vyombo vya maamuzi ❖ Kuwepo kwa ajira za uonevu hususani katika maeneo ya uchumi huria (EPZ) na ongezeko la ajira za vibarua zenye malipo duni. ❖ Kuongezeka kwa ajira za watoto katika mashamba ya chai, mikonge, kahawa na miwa, migodi na kazi za ndani.	❖ Kufanya tafiti na kuzisambaza kwa njia ya machapisho, semina, mikutano. ❖ Kufanya Majadiliano na waajiri na serikali. ❖ Migomo isiyo rasmi ❖ Kutumia shinikizo kwa serikali kupitia mashirikisho huru ya Wafanyakazi duniani , na mashirika ya kimataifa.	❖ Wafanyakazi kushirikishwa zaidi katika sera na mipango ya serikali. ❖ Wafanyakazi kuachwa huru bila kuwekwa chini ya chama chochote cha siasa ama serikali. ❖ Kuundwa kwa vyama huru vya wafanyakazi vya kisekta vya demokrasia zaidi. ❖ Vyama vya Wafanyakazi kuanzisha kampeni na programu maalum za kuondoa ajira za watoto nchini.

KIPINDI (MWAKA) 2000- 2005

MFUMO WA VYAMA VYA WAFANYAKAZI	MFUMO WA KISIASA	MFUMO WA UCHUMINA SERA ZILIZOTUMIKA	MATATIZO KWA WAFANYAKAZI	MBINU ZILIZOTUMIWA NA WAFANYAKAZI KUKABILI MATATIZO	MATOKEO
Vyamavingi vya Wafanyakazi vya kisekta kama vile: A: Vyaa Shiriki vya TUCTA: tuicko cwt, tij, tasu, TUGHE, TRAWU, CHODAWU, TPAWU, TALGWU, TAMICO, RAAWU, COTWU(t) B: Vyama Visivyoshirikishwa TUCTA: dowuta, igwuta, tupse, wameuta, tasiwu, taweta	Vyama vingivya siasa	Mfumo wa uchumi wa soko huria. Unaotekelezwa kwa sera za kurekebisha uchumi, ubinafsishaji wa mashirika ya umma kuvutia wawekezaji toka nchi za nje.	❖ Mazingira duni ya kazi ❖ Mishahara duni ❖ Uhuru wa Wafanyakazi ❖ Uhuru mdogo ukiukwaji wa haki za Wafanyakazi za kuunda am kujiunga na chama chochote cha Wafanyakazi katika baadhi ya sehemu za kazi. ❖ Kutokushirikishwa kikamilifu katika mipango na sera za uchumi na Maendeleo ya nchi. ❖ Uwakilishi duni wa wafanyakazi katika vymbo vya maamuzi. ❖ Upunguzwaji wafanyakazi katika zoezi la ubinafsishaji. ❖ Kungezeka kwa ajira za vibarua. ❖ Ukiukwaji wa Sheria za kazi. ❖ Kufukuzwa kazi ovyo.	❖ Kufanya tafiti na kuzisambaza kwa njia ya machapisho, semina mikutano. ❖ Kufanya Majadiliano na waajiri na serikali. ❖ Migomo isiyo rasmi. ❖ Kutumia shinikizo kwa serikali toka mashirikisho huru ya Wafanyakazi duniani, mashirika ya kimataifa kama vile ILO nna wafadhili (IMF, wb). ❖ Kuwasaidia wafanyakazi walioajiajiri katika sekta isiyo rasmi kwa kuwapatia mafunzo ya ujasiriamali (Enterpreneurs hip) na mikopo midogo na kuwaunganisha katika vyama vya kuweka na kukopa (SACCOS) na vyama vya wafanyakazi. ❖ Kutoa mafunzo ya mbinu za majadiliano, mawasiliano, na ushawishi kwa viongozi wa Wafanyakazi ili wawe wawakilishi na watetezi wazuri wa wafanyakazi.	❖ Kuridhiwa Naa serikali ya Tanzania kwa mikataba ya ILO ya kuruhusu uhuru wa Wafanyakazi kujiunga na chama chochote na kufanya Majadiliano na waajiri (ILO ONV. 87 na 98). ❖ Kushirikishwa kwa Vyama vya Wafanyakazi katika masuala mbalimbali mfano PRSP, Cotonou Agreement. ❖ Kurekebishwa kwa Sheria za kazi. ❖ Kushinda kesi nyingi mahakami zilizoonea Wafanyakazi.

				❖ Kutoa elimu na mafunzo mbalimbali kwa viongozi na Wafanyakazi kuhusu Afya na Usaolama Kazini, Sheria za Kazi, Haki za Wafanyakazi, Jinsia, Uchumi na Sera, n.k.	